CHANGAMOTO

# Wanafunzi wataja mbinu kuondoa kero ya usafiri

**Waandishi Wetu**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz



Baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari jijini Mbeya wakiwa kituo cha daladala wakisubiri usafiri. Changamoto ya huduma hiyo kwa kundi hilo imetajwa kuwa kero kubwa kwao. **Picha na Mpigapicha Wetu**

**Dar es Salaam/Mikoani.** Baadhi ya wanafunzi nchini wameeleza adha wanazokumbana nazo wanapotumia usafiri wa umma, huku wakitaka kuwepo kwa sheria mahsusi itakayolazimisha na kusimamia usafiri kwa wanafunzi.

Februari 4 mwaka huu, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa aliiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) kuwaadhibu madereva na makondakta wa daladala wanaowanyanyasa wanafunzi.

Hata hivyo, wanafunzi hao walisema kwa kuwa nchi inaendeshwa kwa misingi ya kisheria, ni vyema hata usafiri wa wanafunzi ukaongozwa na sheria badala ya kuachwa kwenye miongozo inayotolewa na viongozi mara kwa mara.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Mwananchi jana, wanafunzi kutoka Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Kilimanjaro walisema kutokuwepo kwa sheria kunawafanya waendelee kubaguliwa na kunyanyaswa bila msaada wa kudumu.

Mather Komba, mwanafunzi wa kidato cha sita katika shule moja ya sekondari jijini Dar es Salaam, alisema umefika wakati wa kuundwa kwa sheria itakayosimamia usafiri wa wanafunzi.

"Tunasikia viongozi wakisema kwa mujibu wa sheria, basi hata usafiri wetu uwe kwa mujibu wa sheria. Konda akikataa kutupakia awajibishwe kisheria," alisema mwanafunzi huo.

Alisema tamko la Profesa Mbarawa, kuhusu kulinda haki za wanafunzi lilipaswa kusimamiwa na sheria.

"Bila sheria tutaendelea kuteseka, halafu tunalaumiwa eti tunapenda kukaa vituoni, wakati makondakta wanakataa kutupakia," alilalamika.

Frida Mwakalebela, mwanafunzi wa shule ya sekondari jijini Mbeya, alisema usafiri mgumu ni chanzo cha wanafunzi wengi kuchelewa kufika shuleni na kuathiri mwenendo wao wa masomo.

> **Bila sheria tutaendelea kuteseka, halafu tunalaumiwa eti tunapenda kukaa vituoni, wakati makondakta wanakataa kutupakia."**
>
> Mather Komba, mwanafunzi

Alisema hali hiyo pia huwaathiri kisaikolojia, kwa kuwa mara nyingi hudhalilishwa na kufokewa vituoni.

"Tunabaguliwa kwa sababu ya nauli ya Sh200 tunayolipa. Asubuhi unaweza kukaa kituoni daladala zinakupita, zikisimama zinawabeba watu wazima na sisi tunabaki na hakuna mzazi anayetutetea wote wanatuangalia tu hata tukitukanwa," alisema Frida.

Alisema wakati mwingine hulazimika kulipa hadi Sh500 au kutembea kwa umbali mrefu kutokana na kunyimwa usafiri.

Mwanafunzi mwingine, Tukali Daniel alisema msaada mkubwa kwa wanafunzi hutolewa na madereva wa magari binafsi, huku daladala zikiwachukua wachache au kuwaacha kabisa.

"Wanaruhusu wawili tu wakati tupo wengi. Msaada wetu mkubwa ni watu wenye magari binafsi," alisema.

Mwanafunzi mwingine aliyekataa kutajwa jina alisema shule yao ina usafiri maalumu wa wanafunzi, lakini gharama zake ni kubwa kwa wazazi wengi.

"Ada ya usafiri imepanda kutoka Sh26,000 ambayo tulikuwa tunalipa mwezi uliopita (Januari) hadi Sh36,000 mwezi huu wa pili. Mzazi akishindwa, unabaki kupambana na daladala au kutembea," alisema.

Hali kama hiyo imeripotiwa pia katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na Edward Mroso, mwanafunzi wa kidato cha tatu akisema uhaba wa daladala na gharama kubwa za bajaji zimeongeza mzigo kwa wazazi. "Sasa tunalipa Sh500 hadi Sh700 kwenye bajaji," alisema mwanafunzi huyo.

Sara Mongi alisema waendesha bajaji wengi huwakwepa wanafunzi kwa kuwa nauli yao ni ndogo.

Katika Mtaa wa Relini na Mabogini, wanafunzi wa shule za msingi Azimio, Juhudi na Mandela walisema hukumbwa na changamoto zaidi jioni.

Jijini Mwanza, mwanafunzi Salum Ally alikiri wakati mwingine wanafunzi wenyewe huchangia tatizo kwa kuchagua magari, lakini akasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa utaratibu wa kudumu wa usafiri wa wanafunzi.

Hata hivyo, Upendo Mushi, mwanafunzi wa Sekondari ya Pamba, alisema anahofia ndoto yake ya kufaulu kupotea kutokana na ugumu wa usafiri, akisema hutembea hadi kilomita 13 kwenda na kurudi shule kila siku hali inayomfanya akose hata muda wa kujisomea kutokana na uchovu.

Awali, Profesa Mbarawa alitoa agizo la kuchukuliwa hatua kali dhidi ya madereva na makondakta wanaowanyanyasa wanafunzi.

Agizo hilo lilitokana na barua ya mwanafunzi wa kidato cha kwanza wa Shule ya Sekondari Jangwani, Dar es Salaam, akidai wanafunzi hubaguliwa na makondakta wa daladala kwa kuwa hawalipi nauli kamili.

Waziri huyo alisema Serikali imezielekeza Latra na Jeshi la Polisi kuimarisha usimamizi wa nauli, usalama na staha ya huduma, kuanzisha mipango ya mabasi na mabehewa maalumu ya wanafunzi, sambamba na kuweka namba za bure za kutoa taarifa za unyanyasaji.

CamScanner

Jumamosi February 7, 2026

**Nukuu**



Mtu asiyeweza kubadili mtazamo wa
chochote duniani.

George Bernard Shaw- Julai 26, 1856- No

# Kero za usafiri kwa wanafunzi zifike mwisho

Ni jambo la kusikitisha na linaloumiza dhamira ya jamii kuona kuwa, katika karne hii ya maendeleo na kauli mbiu lukuki za kulinda haki za mtoto, wanafunzi bado wanakabiliwa na manyanyaso ya wazi katika huduma za usafiri wa umma, hususan mijini.

Kero za usafiri kwa wanafunzi si jambo jipya; ni kilio cha miaka nenda rudi ambacho kimekuwa kikisahaulika au kupewa ufumbuzi wa muda mfupi usio na tija. Sasa ni wakati mwafaka kwa kero hizi kufikia mwiko na kukomeshwa kabisa.

Kila siku asubuhi na jioni, wanafunzi wengi hulazimika kupambana na hali ngumu ya usafiri wanapoelekea shuleni au wanaporudi majumbani.

Vilio vyao vimekuwa vya kufanana; kunyanyaswa na makondakta, kuzuiwa kupanda daladala kwa kisingizio cha "hatuwabebi wanafunzi", au kutozwa nauli ya watu wazima kinyume na taratibu zilizopo.

Wapo wanafunzi wanaolazimika kusimama vituoni kwa muda mrefu, wakikosa usafiri kwa sababu tu wamevaa sare za shule.

Wengine hulazimika kulipa zaidi ya uwezo wao au kutembea umbali mrefu ili kuepuka manyanyaso hayo.

Matokeo ya hali hii ni makubwa na yenye kuumiza. Wanafunzi wengi wamekuwa wakichelewa kurejea majumbani, wengine wakifika usiku mwingi hali inayowaweka katika hatari za kiusalama na kiafya.

Baadhi hulazimika kubadili ratiba zao za masomo au shughuli za ziada shuleni ili kuendana na changamoto za usafiri. Kwa namna isiyo ya haki, mzigo wa uzembe na ukatili wa wachache unaangukia mabegani mwa watoto wasiokuwa na hatia, huku ndoto zao za elimu bora zikiwekwa rehani.

Ikumbukwe kuwa wanafunzi ni kundi maalumu linalostahili ulinzi wa ziada. Taifa lolote linalojali mustakabali wake haliwezi kuvumilia kuona watoto wake wakinyanyaswa hadharani kwa maslahi binafsi ya makondakta na madereva wasiozingatia maadili wala sheria.

Tatizo hili limekuwa sugu kiasi kwamba limeonekana kama jambo la kawaida, ilhali si la kawaida wala halikubaliki.

Habari njema, hata hivyo, ni kujitokeza kwa Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa na kutoa kauli nzito kuhusu kero hizi. Hatua yake ya kueleza mikakati mbalimbali, ikiwamo kuitaka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ( Latra) kuwachukulia hatua kali madereva na makondakta wanaowanyanyasa wanafunzi, ni ishara ya matumaini mapya.

Hata hivyo, ni muhimu kusisitiza kuwa tatizo hili halitamalizwa kwa matamko pekee. Historia imetuonyesha kuwa kauli nyingi nzuri zimekuwa zikitolewa, lakini utekelezaji wake umekuwa dhaifu au wa msimu.

Suala la usafiri kwa wanafunzi linahitaji utafiti wa kina ili kubaini chanzo halisi cha tabia hizi, mianya iliyopo katika mfumo wa usimamizi wa usafiri na namna bora ya kuwalinda wanafunzi kwa muda mrefu.

Bila kufanya hivyo, tutakuwa tunapambana na dalili badala ya ugonjwa wenyewe.

Masuluhisho yanayotafutwa yanapaswa kuwa makini na endelevu. Ni wakati wa kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi na ufuatiliaji, ikiwamo adhabu kali na za haraka kwa wanaokiuka sheria, lakini pia elimu kwa madereva na makondakta kuhusu haki za wanafunzi na wajibu wao kwa jamii.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inaweza kuangalia uwezekano wa kuwepo kwa usafiri maalumu au ratiba rafiki kwa wanafunzi, ili kupunguza utegemezi wao kwa daladala zisizofuata taratibu.